

## KINA CHA FIKIRA



KAULI YA WALIBORA

**"Kwa hiyo naungana na Prof Kimani na wengine wanaosema kwamba istilahi elimumtindo labda ni tafsiri kombo kwa vile inajikita hasa katika tasnia ya elimu"**

PROF Kimani Njogu amewasha kiberiti cha moto ambao ulitishia kuteketeza msitu mukubwa alipouliiza hivi karibuni kwa nini istilahi "literary stylistics" imetafsirira eliumtindo na baadhi ya wanataluma.

Unapojaribisha kitu ili kuona matokeo yake yatakuwaje au yatakuwa nini, tunaweza kusema "unatingisha kiberiti ili kuona kama ndani mna njiti" katika Kiswahili cha kisanii. Prof Njogu hakuwa anatingisha tu njiti, ameuliza swali la kuchochea mjadala impevu kuhusu usahihi wa baadhi ya istilahi zinazotumika katika taaluma za Kiswahili. Kama hatuwezi kuanza kusaili baadhi ya istilahi na mikondo na mikabala tutakuwa tunazihini taaluma fursa ya kwenda mbele.

Kiswahili mbele hakiendi pasi na kuuliza maswali yenyе mwelekeo wa kimapinduzi, maswali yanayokaribiana na kufuru. Hatuwezi kuendelea kuafikiana na maneno na istilahi zilizoko na hata kanunu za sarufi kimsobemsobe tu. Sharti tusitawishi tabia ya kusaili na kujisaili. Prof Kimani kauiliza kuna uhusiano gani kati ya istilahi ya Kiswahili elimumtindo na *literary stylistics*?

Nao wachangiaji wakachochewa kutoa maoni mbalimbali yanayokinanza. Kama utanzu wa taaluma, *stylistics* inajishughulisha na matumizi ya mitindo katika kazi za fasihi. Kwa hiyo naungana na Prof Kimani na wengine wanaosema kwamba istilahi elimumtindo labda ni tafsiri kombo kwa vile inajikita hasa katika tasnia ya elimu. Nasema labda kwa vile, kwa baadhi ya wasomi, nadhani Prof Hermas Mwansoko na Prof Kineene wa Mutuso wamo humu, neno la Kiingereza "study" linaweza kutafsirisha kama elimu kwa Kiswahili na wala sio elimu kama kisave cha neno la Klingereza "education" tu.

Ndiyo maana mnajimu anawenza kuelezewa kama mtaalamu wa elimu ya nyota, kabobeza na kutopea (huu uradidi ni mtindo wa Wallah bin Wallah)

# Taaluma ya Kiswahili yahitaji asasi madhubuti kuboresha utumizi wake



kwenye taaluma au elimu (study) ya nyota.

Je, mijadala kama hii itaishia kwenye kumbi la jamii mitandaoni au itaifika asasi mahsusini zinazohusika na kutoa miongozo na maeleko thabiti ya matumizi ya lugha katika taaluma za Kiswahili? Hapa ndipo kwa kweli tunapohitaji Barazala Kiswahili la Taifa linalotenda, lenye meno yanayong'ata (tafsiri mbaya hii, sio?). Upo mwamko mwemwa wa kusailisaili. Mwamko huu si tu katika swali la Prof Kimani Njogu bali katika mambo mengine mengi. Kila mwamko huu ukijiteaza katika taaluma hizi za Kiswahili, ipo haja kujenga utamaduni wa kushirikiana na kushauriana, si kushindana na kuhami-

siana na kufikia mahitimisho yanayojenga taaluma.

Ninahisi taaluma za Kiswahili zimejaa kelele nyingi mno zinazopigwa kiholela na wamba-ngoma kadha wa kadha, kila mmoja aktivitura kwake. Hizi kelele ni nzuri ila zinaonesha kwamba ipo haja kuwa na vyombo vya kuzidhibiti.

Kelele hizi hazipaswi kuanzia na kuishia kwenye kumbi la kijamii mitandaoni. Waama, kelele hizo zinaonesha hamkani si shwari tena na kama asasi zilizopo hazikidhi haja, wakereketwa watajiundi wenywewe asasi mbadala za kimapindukizi na kuchapusha ukuzi wa Kiswahili.